

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

02/08/2021

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

"UGONJWA WA UVIKO- 19 UPO JAMII ISIPUUZE" RC MAKALLA

Ahimiza kuzingatia mwongozo uliotolewa na Wizara ya afya katika kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19

Kusitisha mikusanyiko isiyo ya lazima

Vyombo vya usafiri kuzingatia "Level seat"

Kuwepo kwa maji tiririka na vitakasa mikono katika maeneo mbalimbali ya mikusanyiko

Uvaaji barakoa ni lazima

Mhe Amos Makalla ameyasema hayo baada ya kufanya kikao na kamati ya ulinzi na Usalama cha tathimini ya utekelezaji wa mwongozo wa Wizara ya Afya katika kukabiliana na UVIKO-19 kwa Mkoa wa Dar es Salaam toka alipotoa tamko mara ya kwanza.

Mkuu wa Mkoa amebainisha kuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam yako maeneo tahadhari inachukuliwa vizuri lakini maeneo mengine bado

"Mfano mtu avaa barakoa anapoingia kwenye kivuko au daladala akiwa ndani anavua hiyo sio sahihi ukijikinga wewe unamkinga na mwenzako" Alisema Mhe Makalla

Aidha ifahamike kuwa Mkoa wa Dar es Salaam una idadi kubwa ya watu na muingiliano mkubwa wa watu kila mmoja akichukua taadhari ni rahisi kupunguza kasi ya kuenea kwa ugonjwa huo.

Vilevile Mhe Mkuu wa Mkoa amewataka wakuu wa Wilaya katika maeneo ya kupitia kamati zao za ulinzi na usalama kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa kukabiliana na UVIKO-19.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM